# Kulima na kuvuna mananasi

Kilimo cha mananasi kinadai muda mwingi, uvumilivu na maarifakinadai muda mwingi, uvumilivu na maarifa.  Shughuli za kulima zinaweza kufanywa kwa mikono au kwa kutumia mashine.

## Mahitaji ya ukuaji wa mananasi

Mananasi hukua vizuri kwenye mchanga wenye nyuzi joto 65 hadi 95. Zikipandwa katika maeneo yenye joto lililo chini kuliko hili, uwezekano wa uchungu huongezeka. Zikipandwa katika maeneo yenye joto zaidi ya hili, juu basi uwezekano wa utamu huongezeka.

## Uanzishaji wa shamba la mananasi

Mimea mpya ya mananasi inaweza kukuzwa kutoka kwa mimea ya zamani. Hili linafanywa kwa kutumia njia 2. Kwa kutumia chipukizi ambalo hukua kutokea kwenye msingi wa mmea, au kwa chipukizi linalotokea kwenye ngozi ya tunda.
Chagua nyenzo bora za upandaji. Majani ya mimea iliyotangulia hukatwa ili kuwezesha ukusanyaji wa mbegu.
Ubora wa mbegu hupimwa wakati wa kuzikusanya, na uzito wazo unapaswa kuwa sawa ili kuhakikisha ukuaji sawa wa mananasi.

## Kupanda na kuvuna

Kabla ya kupanda mananasi, unahitaji kufanya maandalizi sahihi ya ardhi.
Kilimo cha mananasi hufanyika bila kutumia kemikali yoyote ambayo inaweza kusababisha uharibifu wa mananasi na mazingira.
Mfumo mzuri wa mifereji ya maji ni muhimu katika kuhakikisha ukuaji sahihi wa mananasi.
Mbegu zinaweza kupandwa kwa mkono, na baada ya kupanda, mananasi lazima yapewe mbolea mara kwa mara.
Kulingana na eneo, nanasi huchukua miezi 13 hadi 16 kutoa tunda.
Kabla ya kuvuna sampuli huchukuliwa na kuchunguzwa ili kupima viwango vya sukari kabla ya kuvuna shamba zima.
Baada ya kuvuna, mananasi huchambuliwa na kufungashwa kwa ajili ya kuuza.